HOTUBA YA MHESHIMIWA JAJI KIONGOZI WAKATI WA UFUNGUZI WA MAFUNZO KWA NAIBU WASAJILI NA HAKIMU WAKAZI WAFAWIDHI WA MAHAKAMA ZA HAKIMU MKAZI KATIKA UKUMBI WA KITUO JUMUISHI CHA MASHAURI YA NDOA NA MIRATHI TEMEKE TAREHE 12/12/2023.

Mhe. Jaji Salma Maghimbi Jaji Mfawidhi DSM

Mhe. Jaji Asina Omari, Kaimu Jaji Mfawidhi Temeke

Mhe. Jaji Shamilla Sarwati Jaji wa Mahakama Kuu Temeke

Dkt. Angelo Rumisha, Jaji wa Mahakama KUU masjala Kuu na Mkuu wa Kitengo cha Maboresho JDU,

Prof. Elisante Ole Gabriel, Mtendaji Mkuu wa Mahakama,

Mhe. Sylivester Kainda, Kaimu Msajili Mkuu,

Bw. Victor Florence Kategere, Mtendaji Mahakama ya Rufani,

Mhe. Projestus Kahyoza, Kaimu Msajili wa Mahakama Kuu,

Bw. Leornard Magacha, Mtendaji wa Mahakama Kuu Kanda

Bi. Mary Shirima, Mtendaji Mahakama Kuu Divisheni,

Wahe. Naibu Wasajili mliopo,

Watendaji wa Mahakama mliopo,

Wakurugenzi na Wakuu wa Idara na wakurugenzi wasaidizi mliopo,

Sekretarieti ya Mafunzo haya,

Ndugu wanahabari,

Mabibi na mabwana.

Mahakama ya Tanzania……

Awali ya yote nianze kwa kumshukuru mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia uhai na kutukutanisha leo tukiwa salama. Pili, nimshukuru sana Mheshimiwa Jaji Mkuu kwa kutoa kibali cha kufanyika kwa mafunzo haya. Tatu, nitumie fursa hii kuwapongeza wote mlioapishwa kuwa Naibu Wasajili pamoja na Mahakimu Wakazi Wafawidhi ambao jana mmepatiwa nyenzo muhimu za kufanyia kazi. Binafsi nikiri kuwa utendaji kazi mzuri, weledi na uadilifu wenu mlipokuwa Mahakimu, ni mambo yaliyowafanya muaminike na leo mmefikia hatua hii ya kuwa viongozi, hongereni sana. Daima msikubali kurudi nyuma. Mna majukumu mazito yanayowasubiri ninyi kwa utekelezaji. Nne, nitumie fursa hii pia kushukuru kitengo cha maboresho (JDU) chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Jaji Dkt. Angelo Rumisha, Mahakama pamoja na kitengo cha mafunzo kwa kuandaa na kuhakikisha mafunzo haya yanafanyika.

Wahe wasajili na mahakimu wakazi wafawidhi, mafunzo mtakayopatiwa takribani wiki nzima yamelenga kuwawezesha kujifunza, kujikumbusha na kubadilishana uzoefu kuhusu majukumu mapya

mnayokwenda kuyatekeleza katika kanda na vituo mtakavyopangiwa. Mafunzo haya yatawanufaisha kwa kupata uwezo, uzoefu, ujuzi na umahiri katika utelekezaji wa majukumu yenu ya kila siku. Nimejulishwa kuwa mafunzo haya yatawezeshwa na watoa mada wenye uzoefu mkubwa na hivyo watawasaidia kuwapa uzoefu wao katika nyanja tofauti za utendaji kazi wenu. Kwa namna mafunzo haya yalivyoandaliwa yatamwezesha kila mmoja wenu kushiriki ipasavyo ama kwa kuchangia mada au kuuliza maswali kwa kadri itakavyowezekana, lengo likiwa kumpa kila mmoja wenu uelewa wa pamoja juu ya majukumu yenu mapya. Achane ule utamaduni wetu wa kukaa kimya na kuhofu. Zungumzeni ulizeni ondokeni hapa mkiwa mnajua silaha kwa maana ya nyenzo tulizo nazo na jinsi ya kuzitumia. Ninaamini kuwa mtakuwa watulivu na wasikivu muda wote wa mafunzo. Aidha, mafunzo haya, ninayaona kuwa ni mwanzo mzuri wa ushirikiano baina yenu, watumishi, viongozi na wadau wakati wa utekelezaji wa majukumu yenu.

Wahe wasajili na mahakimu wakazi wafawidhi, nianze kwa taarifa nzuri. Mtakumbuka mwaka huu taasisi huru ya REPOA ilifanya utafiti juu ya kuridhika kwa watumiaji wa Huduma za Mahakama (**Court User's Satisfaction Survey Report, 202**3), matokeo ya utafiti huo, yanaonyesha kuwa kiwango cha Watumiaji wa huduma zinazotolewa na Mahakama kimepanda kutoka **78%** mwaka, **2019** hadi **88%** mwaka huu wa **2023.**

Hata hivyo mtakumbuka jana nilipopata nafasi ya kuwasalimia, nilizungumza kwa ufupi kuhusu mambo yanayowakabili mbele yenu. Nilitaja mawili. Kwanza ni eneo la utekelezaji wa amri za mahakama na pili ni wajibu wenu katika kujenga imani ya umma kwa taasisi yetu na kuimarisha ushirikiano na wadau wetu. Nilisema eneo hili linalalamikiwa zaidi. Maeneo haya yanawahitaji ninyi kwenda kuyaboresha ili taarifa ijayo ya REPOA iendelee kupanda. Kumekuwa na khofu katika eneo la utekelezaji wa hukumu kwa sababu ya mbalimbali ikiwemo kulalamikiwa. Ninataka ninyi mwenye kuifanya kazi hiyo bila khofu. Mkatimize wajibu wenu kwa mujibu wa viapo vyenu. Msihofu kuhusu malalamiko ilimradi mmetenda haki. Kazi ya kutoa haki siku zote inakaribisha kulalamikiwa. Lakini lalamiko lolote linalotokana na kutimiza wajibu wa haki ni baraka na lalamiko linalotokana na kupindisha haki ni laana. Kama mnaniskia na kunielewa, chagueni baraka.

Wahe wasajili na mahakimu wakazi wafawidhi, ninyi ni wasimamizi wa masjala zetu za Mahakama nchini. Kupitia mafunzo haya mtaelezwa mambo mengi ya msingi kuhusu usimamizi wa masjala za Mahakama na utaoji huduma za Mahakama. Kama mnavyo jua, mfumo wa Usimamizi wa Mashauri ulishaanza kufanya kazi kupitia mafunzo hayo tumieni fursa hiyo kuufahamu vizuri mfumo huu kwa kuwa mnakwenda kuutelekeza kwa vitendo. Mbali na mfumo huo, pia mtapata nafasi ya kufahamu mfumo tanzlii ambao unawezesha umma kupata habari hasa maamuzi mbalimbali. Aidha, wakati wa mafunzo haya, mtawezeshwa kuifahamu miongozo ya ukaguzi wa

Mahakama na magereza, majukumu ambayo mnakwenda kuyatekeleza katika maeneo yenu.

Katika mafunzo haya mtafundishwa pia kuhusu ushughulikiaji wa malalamiko ya wananchi dhidi ya huduma zinazotolewa. Aidha, mtafundishwa taratibu za kufanya uchunguzi wa tuhuma dhidi ya maafisa Mahakama waliochini yenu. Tumieni fursa hii kujifunza utaratibu wa kufanya kazi hiyo. Kama viongozi, mnawajibika kudhibiti malalamiko katika maeneo yenu na pale yanapojitokeza yashughulikiwe na kwisha badala ya kuacha walalamikaji wakihangaika huku na kule ofisi baada ya ofisi kwa kutotatuliwa kero zao.

Wahe wasajili na mahakimu wakazi wafawidhi, Kama mnavyofahamu dunia ya sasa inaongozwa na TEHAMA. Kwa hiyo, mwelekeo wa Mahakama ni kuwa ifikapo mwaka, 2025 tuwe na Mahakama Mtandao isiyotumia karatasi. Ni matarajio yangu kuwa baada ya mafunzo haya, mtaenda kusimamia utekelezaji wake hasa mfumo wa Usimamizi wa Mashauri na baadaye mfumo wa kutafsiri na kurekodi. Aidha, kupitia mafunzo haya mtatafakari namna nzuri wa kutambua mashauri ya mlundikano (backlog cases) na kuyawekea mkakati wa uondoshaji wake kwa njia ya vikao maalum yaani *special clean up sessions* na kudhibiti mlundikano kujitokeza (back stopping of backlog cases) katika maeneo yenu.

Kupitia mafunzo haya mtakumbushwa suala la uzingatiaji wa maadili katika utoaji haki na pia kuwasimamia maafisa Mahakama wengine kuzingatia

maadili ya kazi. Pamoja na mambo mengine, mtakumbushwa kufanya kazi kwa kuzingatia Katiba, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali.

Wahe wasajili na mahakimu wakazi wafawidhi, mtakumbuka jana wakati wa uapisho wenu, Mheshimiwa Jaji Mkuu, alitoa hotuba nzuri ambayo mtapaswa kuisoma na kuitafakari kwa kina katika kipindi hiki cha mafunzo, mtapaswa kuyatekeleza na kuyatolea taarifa masuala muhimu yaliyoelezwa katika hotuba hiyo. Ninyi ni watu muhimu katika maboreshaji ya huduma za utoaji haki kupitia Mipango Mkakati na Programu za Maboresho ya Mahakama. Jaji Mkuu aliwafananisha ninyi na engine. Mimi nawaona wasajili na mahakimu wafawidhi kama moyo wa mahakama. Kwa umuhimu wenu msipofanya kazi inavyostahiki, mahakama haiwezi kuwa hai. Mafanikio yetu yatategemea sana ninyi mnafanyaje kazi. Kwa hiyo mtalazimika kuitekeleza kwa vitendo Dira ya Mahakama ya Tanzania ya utoaji haki kwa wakati na kwa watu wote (Timely and Accessible Justice for all).

Umuhimu wenu kwa mahakama unatokana na majukumu makubwa ambayo sheria na miongozo mbalimbali imeweka kwenu. Naibu Msajili au Hakimu Mkazi Mfawidhi ana wajibu mkubwa wa kuongoza watumishi wengine wa mahakama katika eneo lake lakini pia ana wajibu wa kuwa Daraja kati ya

mahakama na wadau wetu wengine ikiweme serikali bunge na umma kwa ujumla. Ninyi ni viongozi na Kiongozi wa mahakama anapaswa kuwa na sifa za kimuundo lakini pia anatarajiwa kuwa sifa za ziada. Kiongozi wa mahakama anapaswa kujua wajibu wake. Atambue yeye kama Naibu msajili au hakimu mfawidhi ana majukumu gani. Awe na check list inayomwezesha kujipima na kujua kila siku amefanya nini. Checklist hiyo inaanzia kwenye mpango mkakati wetu.

Kiongozi wa mahakama anapaswa kujipima yeye mwenyewe kabla hajapimwa na umma au viongozi wa juu yake. Ni lazima ajue kwa asili ya kazi yake atapimwa tu na kipimo chake kikubwa ni kwa umma anaouhudumia.

Kiongozi wa mahakama, anapaswa kuwa na mfano wa maadili ndani na nje ya mahakama. Kila wakati anapaswa kujitazama na kujiuliza ikiwa anachotenda kinaipa sifa nzuri mahakama au kinaichafua.

Kiongozi wa mahakama anapaswa kuwa mwenye busara, heshima, adabu, mvumilivu na mwenye lugha nzuri. Kiongozi wa mahakama hapaswa kuwa

mwenye kiburi, hasira zivukazo mpaka. Hapaswi kujivuna na kujiona yeye ni bora kuliko wengine. Kumbukeni miongoni mwa mambo yaliyowafikisha hapa ni maoni ya wananchi mliowahudumia. Kama mtabadilika, mkalewa sifa za ubosi, wananchi wale wale waliotoa maoni mazuri juu yenu, ndio watakaowaangusha.

Kiongozi wa mahakama sio tu hapaswi kula rushwa, bali hapaswi hata kuhisiwa amekula rushwa. Kiongozi wa mahakama ni mfano wa tabia njema unaopaswa kuigwa na watumishi wenzake na kuzungumwa vizuri na umma. Kiongozi wa mahakama sio kikwazo kwa walio chini yake kukua. Kiongozi wa mahakama anapaswa kuwa mlezi anayeibua na kukuza vipaji vya walio chini yake.

Kiongozi wa mahakama, ni yule ambaye ukimpima utaona yuko juu ya viwango vya kawaida. Kiongozi wa mahakama sio mtu wa kulalamika. Ni mtu anayetafuta majibu kwa changamoto zinazoikabili ofisi yake (problem solver).

Kiongozi wa mahakama ni mtu anayewaunganisha watumishi wote wa mahakama. Kwa namna hiyo Kiongozi wa mahakama si mbaguzi kwa namna yoyote. Sio yule anayesema huyo ni judicial officer ni mheshimu na huyu sio judicial officer aniheshimu. Kiongozi wa mahakama, anapaswa kuheshimu watu wote na anapaswa kuwa na hofu ya Mungu kwa imani yake. Hata kama haamini uwepo wa Mungu, awe na mfano wa huruma ya Mungu. Hatuwezi kuwa na kiongozi katili ambaye hawajali watu.

Wahe wasajili na mahakimu wakazi wafawidhi, ninapokwenda kuhitimisha na kabla ya kufungua rasmi mafunzo haya, niwakumbushe kwamba kuwa naibu msajili au hakimu mkazi mfawidhi haimaanishi mmepewa kibali cha kuacha kusikiliza mashauri. Kwa mfano kuna waraka zinazowataka naibu wasajili kusikiliza mashauri huku mkiendelea na majukumu yenu ya kiutawala. Waraka husika umeainisha hadi idadi ya chini ya mashauri mnayopaswa kumaliza kwa mwaka. Kazi yenu ya uhakimu haifi kwa kuwa wasajili. Misingi ile ile ya uhakimu inapaswa kuwaongoza mnapotekeleza majukumu yenu nayo ni kuhakikisha mnaishi viapo vyenu na hapa ningependa kurejea maneno ya Dr. Ndika, Jaji wa Mahakama ya Rufani ambaye kwa nyakati tofauti amekuwa akisisitiza yafuatayo; ***Moja****, Kazi*

tunayofanya iwe Uhakimu, Usajiri au Ujaji sio ajira wala wito. Ni dhamana tuliyopewa na Watanzania chini ya Katiba yetu. Kwa sababu hiyo tunawajibika kutenda kazi yetu ya utoaji haki kwa kufuata Kanuni zetu za Maadili. Tuna wajibu wa kuviishi viapo vyetu vya kutoa haki bila huba, upendeleo, hofu au chuki. ***Mbili,*** *kazi ya utoaji haki inafanywa hadharani na matokeo yake ambayo ni maamuzi tunayoyatoa yanawekwa hadharani. Hakimu au Jaji hawezi kujitetea baada ya kutoa maamuzi yake hasa pale hukumu hiyo inapokuwa na kasoro. Hivyo, tuzingatie kuwa hukumu tutakazozitoa ziwe na ubora na zenye kukidhi viwango ili ziweze kujieleza kwa ufasaha. Tutoe hukumu ambazo zitajitetea zenyewe.* ***Tatu,*** *kazi ya utoaji haki ni ngumu sana na pia ina lawama hasa kutoka kwa wadaawa walioshindwa. Hivyo tunatakiwa kuwa wavumilivu sana. Tena sana. Tusikate tamaa tunapotupiwa lawama hasa kwenye mitandao ya kijamii. Lakini pia tukubali kukosolewa pale inapostahili.* ***Nne,*** *ni wajibu wa kila mmoja kutambua kuwa yeye ni kiongozi na kwamba katika kufanya kazi na wenzake azingatie umuhimu wa urafiki, kuheshimiana na kushirikiana* ***(friendliness, courtesy, mutual respect and pride in the group)****. Kila mmoja afanye kazi kwa kutambua na kuthamini uwezo na mchango wa mwenzake. Hii ndio dhana ya collegiality (ushirikiano)...*

Haya ni maneno muhimu na ningependa kila mmoja wenu ayazingatie na kuyafanyia kazi.

Wahe Naibu Wasajili na Mahakimu Wafawidhi, ninapohitimisha niwaachie kazi za kuanzia:

1. Jana mlimskia mhe Jaji Mkuu akisisitiza kuhusu mpango wa "kudigitilize" nyaraka zote za mahakama. Ili kutekeleza alichokisema, nimeelekeza mpitishwe kwenye mpango kazi wa Kudijiti Nyaraka. Nataka muelewe vizuri majukumu ya kila aliyetajwa kuhusika na Utekelezaji. Uteuzi wenu umeendana na kipindi cha majaribio au probation period. Katika kipindi hicho cha Probation, Kila mmoja wenu atapswa kuniletea taarifa kila mwezi nini amefanya katika hili eneo hili muhimu la kudijiti. Nitapenda kupata kutoka kwenu taarifa za changamoto ili zitafutiwe ufumbuzi.

2. Mtapitishwa kwenye Mfumo wa unukuzi na kutafsiri. Nataka muuelewe mfumo huo na kila mwezi wa probation mnitumie taarifa kuhusu ufanyaji kazi wa mfumo huo faida zake na changamoto zinazojitokeza.

Tutatumia Changamoto mtakazoibua kuufundisha mfumo kwa lengo la kuuboresha. (Hii ni kwa wale ambao tayari mfumo huu umefungwa kwenye kanda au vituo vyao). Kwa wale ambao mfumo huu haujafungwa katika vituo vyao, naelekeza watenge wiki moja katika kipindi cha miezi 6 ijayo waende kwenye vituo vyenye mfumo huo kujifunza na kutoa taarifa kama nilivyoelekeza. (Hawa watatoa mara moja)

Ili kutekeleza mambo hayo mawili, ofisi ya Msajili Mkuu kupitia kurugenzi ya mashauri (DCM) iandae utaratibu wa uwasilishwaji wa taarifa husika na namna zitakavyonifikia.

Baada ya kusema hayo, nirudie kuwapongeza sana. N sasa ni fahari kubwa kwangu, kutamka kuwa Mafunzo haya elekezi kwa Waheshimiwa Naibu wasajili na Makimu Wakazi Wafawidhi wa Mahakama za Hakimu Mkazi yamefunguliwa rasmi.

Asanteni kwa kunisikiliza na ninawatakia mafunzo mema.